

Benki za Maendeleo ya Shughuli Mbalimbali

Benki za Maendeleo ya Shughuli Mbalimbali ni mashirika yanayopeana msaada wa kifedha na wasia wa kitaalamu kwa shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi zinazoendelea. Neno Benki Maendeleo ya Shughuli Mbalimbali (**MDB**) haswa humaanisha Mshikano wa Benki ya Dunia na mabenki manne ya sehemu za dunia:

- ▶ [The African Development Bank](#) [Benki ya Afrika ya Maendeleo]
- ▶ [The Asian Development Bank](#) [Benki ya Asia ya Maendeleo]
- ▶ [The European Bank for Reconstruction and Development](#) [Benki ya Ulaya ya Marekebicho na Maendeleo]
- ▶ [The Inter-American Development Bank Group](#) [Mshiko wa Benki ya kati-ya-Amerika ya Maendeleo]

Benki hizi zina sifa ya kuwa na uwanachama mkubwa unaojumlisha nchi zinazoendelea zinazo pata mikopo na nchi zilizoendelea zenye kutoa mikopo. Na uwanachama hauishii katika nchi wanachama wa benki ya maendeleo ya sehemu ya nchi. Kila benki ina hadhi yake yenyewe ya kisheria na ya uendeshaji-lakini yenye mamlaka sawa na idadi ya kutosha ya wamiliki wa pamoja, MDB hizi hudumisha ushirikiano wa hali ya juu.

MDB hizi hupeana fedha za maendeleo kwa njia zifwatazo:

- Mikopo ya mda mrefu sambamba na kiasi cha riba cha wakati huo. Ili ziweze kupeana hii mikopo MDB hukopa katika masoko ya kimataifa ya fedha na kukopesha serikali zinazokopa katika nchi zinazoendelea.
- Mikopo ya mda mrefu zaidi (kawaida inaitwa karadha), yenye riba ya kiasi cha chini zaidi ya kile cha soko. Mikopo hii hufadhiliwa kwa michango ya moja kwa moja katika nchi wafadhili.
- Kufadhili kwa Karadha pia haufanywa na baadhi ya MDB, hususa kwa masaada wa kifundi, huduma ya kupeana mawazo ama uandalizi wa miradi.

Benki nyengine kadhaa na mifuko inayopeana mikopo kwa nchi zinazoendelea zinafahamika pia kama mashirika ya maendeleo mbalimbali, na kawaida hujumuishwa pamoja kama **other Multilateral Financial Institutions (MFIs) [Mashirika Mengine ya Kifedha za Shughuli Mbalimbali]**. Yanatofautiana na MDB kwa kuwa umiliki/uwanachama mdogo zaidi ama katika kushughulikia kwake sekta ama miradi ya hususa. Kati yake ni:

- [The European Commission \(EC\)](#) [Tume ya Ulaya] na [The European Investment Bank \(EIB\)](#) [Benki ya Ulaya ya Uwekezaji]
- [International Fund for Agricultural Development \(IFAD\)](#) [Hazina ya Kimataifa la Maendeleo ya Ukulima]
- [The Islamic Development Bank \(IDB\)](#) [Benki ya Kiislamu ya Maendeleo]
- [The Nordic Development Fund \(NDF\)](#) [Hazina ya Nordic la Maendeleo] na [The Nordic Investment Bank \(NIB\)](#) [Benki ya Nordic ya Uwekezaji]
- The OPEC Fund for International Development (OPEC Fund) [Hazina ya OPEC ya Maendeleo ya Kimataifa]

Baadhi ya **Sub-Regional Banks [Benki za Sehemu za Nchi]**, zilizobuniwa kwa madhumuni ya maendelo, zinafahamika pia kama benki za shughuli mbalimbali kwa sababu zina milikiwa na kundi la nchi (kwa kawaida wanachama wanaopokea mikopo na wala siyo wanaopeana mikopo). Kati yao ni benki kama: Corporacion Andina de Fomento (CAF) [Ushirika wa Andea wa Maendeleo]; [Caribbean Development Bank \(CDB\)](#) [Benki ya Caribbean ya Maendeleo];

[Central American Bank for Economic Integration \(CABEI\)](#) [Benki ya Amerika ya Kati ya Umoja wa Uchumi]; [East African Development Bank \(EADB\)](#) [Benki ya Afrika Mashariki ya Maendeleo]; [West African Development Bank \(BOAD\)](#) [Benki ya Afrika Magharibi ya Maendeleo].